



Yeyote atakaetubebea silaha dhidi yetu, si mionganoni mwetu

Imepokewa Kutoka kwa Abuu Mussa Al-Ash'ary-Radhi za Allah ziwe juu yake- kutoka kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- amesema: "Yeyote atakaetubebea silaha dhidi yetu, si mionganoni mwetu".

[Sahih] [Wamekubaliana Bukhaari na Muslim]

Anamtahadharisha Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- yeyote atakayebeba silaha dhidi ya waislamu, kwa ajili ya kuwatisha au kuwapora, atakayefanya hivyo pasina haki, atakuwa ametenda kosa kubwa na dhambi mionganoni mwa madhambi makubwa, na atakuwa kastahiki kemeo hili kali.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/2997>

النّجاة الخيريّة
ALNAJAT CHARITY



لجنة الدعوة الإلكترونية
EDC E-Da'wah Committee